# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA SABA

**08 FEBRUARI, 2023**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 08 FEBRUARI, 2023

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**104. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kutatua changamoto ya uhaba wa Walimu katika Shule za pembezoni.

**105. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza Mpango wa Matumizi bora ya Ardhi ili kuondoa migogoro ya Wakulima na Wafugaji katika Wilaya ya Kilwa.

**106. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mbinga Luwaita kupitia Mradi wa *Agri connect* kwa kiwango cha lami.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**107. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha Taasisi ya TAKUKURU katika uwajibikaji wake.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**108. MHESHIMIWA MOHAMMED JUMAH SOUD (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa kuanzisha Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi kusaidia kupambana na athari za mabadiliko ya Tabianchi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**109. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kuwapatia Wananchi maeneo ya kulima kutoka kwenye mapori na Hifadhi ambazo hazina wanyama kwa sasa.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**110. MHESHIMIWA BONIVENTURA DESTERY KISWAGA (MAGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kuna mpango gani wa kuweka taa za barabarani katika Miji ya Magu, Kisesa, Nyanguge, Lugeye na Ilungu.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**111. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILU ZODO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha Wakulima wa zao la Mwani ili kuongeza tija.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**112. MHESHIMIWA SALIM MUSSA OMAR (GANDO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza magari ya kisasa ya zimamoto.

**WIZARA YA MAJI:**

**113. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti kuhama kwa Mto Ruvu – Kibaha ili kuzuia uharibifu wa mashamba na miundombinu ya Reli ya SGR.

**WIZARA YA AFYA:**

**114. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje kutoa elimu juu ya Ugonjwa wa Fistula.

**115. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itafanya upanuzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro.

**WIZARA YA KILIMO:**

**116. MHESHIMIWA DUNSTAN LUKA KITANDULA (MKINGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mwakijembe pamoja na Bwawa la kukinga maji.

**WIZARA YA NISHATI:**

**117. MHESHIMIWA NICHOLAUS GEORGE NGASSA (IGUNGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Kata za Mtungulu, Mwamashiga, Isakamaliwa, Kining'inila na Kinungu zitapatiwa umeme.

**118. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Kijiji cha Kanonge Kata ya Nsimbo kitapelekewa umeme wa REA.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

**119. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA (KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni vigezo gani Serikali inavitumia kusamehe Kodi ya *VAT* kwa viwanda mbalimbali nchini katika kuleta usawa kwa wote.

**WIZARA YA MADINI:**

**120. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni madini aina gani yanapatikana katika Mkoa wa Rukwa na katika maeneo gani.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**121. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali inawasaidiaje Wajane kuondoa mila potofu zinazomkandamiza Mwanamke kwenye suala la mirathi.

**IV. HOJA ZA KAMATI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**DODOMA**
**08 FEBRUARI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**